

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA



MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA KWANZA KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W) TAREHE 12/11/2021

AGENDA

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha mihtasari wa vikao vilivyopita
4. Yatokanayo
5. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia Mwezi Septemba 2021
6. Taarifa ya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za mradi wa SRWSS Tsh 272,830,000/=
7. Maombi ya kubadili matumizi ya fedha kiasi cha Tsh. 50,065,416.33 ikiwa ni fedha iliyobaki baada ya ununuzi wa gari ya mkurugenzi.
8. Mapokezi ya fedha Tshs 1,671,872,380/= na kuwasilisha mgawanyo wa fedha kwa vyumba vya madarasa ya shule za msingi , sekondari, bweni la wanafunzi wenyewe mahitaji maalum uchimbaji wa kisima kirefu na miundo mbinu ya kunawia mikono.
9. Taarifa za Idara na vitengo Robo ya Kwanza Julai – Septemba 2021
 - (a) Utawala na Utumishi
 - (b) Taarifa ya Miradi ya Maendeleo
 - (c) Ukaguzi wa Ndani
 - (d) Manunuzi
 - (e) Sheria
 - (f) Uchaguzi
 - (g) TEHAMA
10. Mengineyo
11. Kufunga Kikao.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

- | | |
|----------------------------|---------------------------------------|
| 1. Mhe. Peter W. Nyerere | - Mwenyekiti H/W Butiama - Mwenyekiti |
| 2. Ndg. Patricia R. Kabaka | - Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu |
| 3. Mhe. Bhoke Ngurube | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Juma M. Sendi | - Makamu M/kiti |
| 5. Mhe. Willy B. Nyamtiga | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Daudi C. Kisangure | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Paul W. Meha | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Magina M. Nyauko | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Nyagheti J. Adam | - Mjumbe |

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

- | | |
|---------------------------|------------------------|
| 1. Mhe. Jumanne A. Sagini | - Mjumbe – Kwa taarifa |
|---------------------------|------------------------|

WAJUMBE (WATAALAM) WALIOHUDHURIA

- | | |
|------------------------------|----------------------------------|
| 1. Ndg. Jobu Ezekia | - Kny; Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 2. Ndg. Deusdedit Kalaso | - Mganga Mkuu (W) |
| 3. Ndg. Robert Makendo | - Afisa Manunuzi |
| 4. Ndg. Leonard Lukawe | - Mweka Hazina (W) |
| 5. Ndg. Alphonse Mlewa | - Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 6. Ndg. Chacha Megewa | - DEO (S) |
| 7. Ndg. Neema Musira | - Kaimu A/Maendeleoyajamii (W) |
| 8. Ndg. Edward Mturi | - Afisa Mifugo/Uvuvi (W) |
| 9. Ndg. Revocatus Lutunda | - Afisa Kilimo (W) |
| 10. Ndg. Leopold Constantine | - Mratibu TASAF |
| 11. Ndg. Julius Wambura | - Afisa TEHAMA |
| 12. Ndg. Sogone R. Wambura | - Kaimu A/Uchaguzi |
| 13. Ndg. Kedmon Chipanyanga | - A/Maliasili Ardhi na Mazingira |
| 14. Ndg. Wumbe E. Harun | - Mhasibu Mapato |
| 15. Ndg. Eunice Makere | - DEO (P) |
| 16. Ndg. Karani Ruhumbika | - Kaimu Afisa U/Mazingira |
| 17. Ndg. Enock N. Warioba | - Mwandishi wa Mikutano |

KUMB NA KFUM/04/18/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:03 asubuhi na kuwakaribisha wajumbe kikaoni. Alisisitiza umoja na ushirikiano ili kuleta maendeleo kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

KUMB NA KFUM/04/19/2021/2022 KUSOMA NA KUTHIBITISHA M1HTASARI YA VIKAO VILIVYOPITA

Mihtasari ya vikao vya tarehe 20/09/2021 na Tarehe 22/09/2021 iliwasilishwa mbele ya kikao na kupokelewa. Iliwekewa saini kama kumbukumbu sahihi.

KUMB NA KFUM/04/20/2021/2022 YATOKANAYO

1. UTOAJI RISITI MINADANI

Wajumbe wa kikao walisisitiza utoaji risiti moja kwa kila anayechinja badala ya kutoa risiti moja kwa kundi la wafanyabiashara waliochinja mifugo mnadani.

Wajumbe wa kikao walisisitiza kuwa kuwekwe utaratibu madhubuti katika kununua bando kwa ajili ya kukusanya mapato badala ya utaratibu uliobainishwa kuwa wakusanyaji wa mapato wanajinunulia bando wanapokuwa wanatekeleza zoezi la ukusanyaji wa mapato.

2. CHANGAMOTO ZA MASHINE MINADANI

Wajumbe wa kikao baada ya kuona changamoto mbalimbali za mashine za kukusanya mapato na kutoshuka kwa miamala kunakopelekea wakusanyaji kupaswa kubaki na fedha za makusanyo kwa muda mrefu kikao kiliazimia kuwa Afisa Tehama awepo kila mnada kwa ajili ya kushughulikia na kutatua changamoto zinazoibuka wakati wa ukusanyaji mapato.

Aidha wajumbe walisisitiza sana suala la kuweka mazingira safi katika minada ili kuepuwa magonjwa ya mlipuko.

KUMB NA KFUM/04/21/2021/2022 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI SEPTEMBA 2021

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kupokelewa. Akiwasilisha taarifa hiyo Mweka Hazina (W) alisema kuwa, kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Septemba 2021 Halmashauri imekusanya kiasi cha **Tshs. 322,114,280.29** sawa na asilimia **21** ya lengo la makusanyo kwa mwaka kutokana na mapato ya ndani.

Kuhusiana na changamoto ya wafanyabiashara ambao hawana vitambulisho vya wajasiriamali wakati wanafanya biashara katika maeneo ya minada wajumbe walisisitiza kuwa suala hili lipelekwe kwenye kamati ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Wakichangia kwa nyakati tofauti wajumbe wa kamati ya fedha walisisitiza ofisi ya mkurugenzi mtendaji (W) kuona na kupunguza orodha ya watumishi wanaokwenda minadani kusimamia mapato na kusema kuwa orodha hiyo ni kubwa na inapaswa kuangaliwa upya.

Wajumbe waliazimia kuwa ofisi ya Mweka Hazina itenganishe mapato kutokana na stendi mbili za kiabakari na magunga badala ya kuweka kwa ujumla.

KUMB NA KFUM/04/22/2021/2022 MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA KIASI CHA TSH. 50,065,416.33 IKIWA NI FEDHA ILIYOBAKI BAADA YA UNUNUZI WA GARI YA MKURUGENZI

Taarifa hiyo iliwasiihwa na kupokelewa. Akiwasilisha taarifa hiyo Afisa mipango alisema kuwa Idara inaomba kutumia kiasi tajwa hapo juu kwa ajili ya ununuizi wa pipipiki 8 aina ya Yamaha kwa ajili ya kuboresha shughuli za makusanyo ya maduhuri ya serikali na kuboresha huduma za ugani kwa wakulima pamoja na kufanya matengenezo ya magari ili kukabili ana changamoto za usafiri Aidha aliongeza kwamba pipipiki hizo zitagawanywa na kamati ya fedha katika idara mbalimbali baada ya kuleta Halmashauri.

Kikao kilipitisha maombi hayo kwa utekelezaji zaidi.

KUMB NA KFUM/04/23/2020/2021 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 1,671,872,380/= NA KUWASILISHA MGAWANYO WA FEDHA KWA VYUMBA VYA MADARASA YA SHULE ZA MSINGI , SEKONDARI, BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM UCHIMBAJI WA KISIMA KIREFU NA MIUNDO MBINU YA KUNAWIA MIKONO.

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha jumla ya Tshs 1,671,872,380/= zikiwa na mchanganuo wa kutekeleza miradi ifuatayo.

1. Ujenzi wa vyumba 72 vya madarasa katika shule 19 za sekondari kiasi cha Tshs. 1,440,000,000/=
2. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa katika shule shikizi za msingi 3 kiasi cha Tshs 120,000,000/=
3. Ujenzi wa bweni 1 la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Madaraka kiasi cha Tsh 80,000,000/=
4. Uchimbaji wa kisima kirefu na ujenzi miundo mbinu ya kunawia mikono katika shule ya msingi Nyamisisi kiasi cha tshs. 31,872,380/=

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuelekeza utekezaji ufanyike kwa wakati na ubora aidha walipongeza serikali kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

KUMB NA KFUM/04/24/2020/2021 TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA KWANZA 2021/2022

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kupokelewa. Wajumbe wa kamati ya fedha walijadili na kuona umuhimu wa kuchukua eneo linalomilikiwa na Nd. Gimunta (ziroziro) na kuazimia kwamba Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi, wenyeviti wa kamati za kudumu, Afisa mipango, Afisa ardhi na mazingira wakutane na mmiliki huyo na kumweleza nia ya Halmashauri kuchukua eneo hilo na kufanya uwekezaji.


6. TAARIFA YA KITENGO CHA TEHAMA.

Taarifa hiyo iliwasilishwa na kupokelewa.

Wajumbe walisisitiza kupata taarifa ya mashine zinazokusanya mapato katika Halmashauri ya wilaya ya Butiama. Aidha wajumbe walitaka kujua ni kwa kiasi gani kitengo kimeshughulikia suala la uwekaji benki fedha za makusanyo. Akijibu suala hili Afisa TEHAMA alisema kuwa changamoto hiyo imetatuliwa na fedha za makusanyo zinatolewa control namba na kuwekwa benki kwa wakati.

KUMB NA KFUM/08/72/2020/2021 KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 10:42 jioni na kuwashukuru wajumbe na wataalam kwa ushiriki wao. Alitoa tangazo la kuanza kutolewa huduma ya X - Ray katika hospitali ya wilaya ya Butiama na kuongeza kuwa itaboresha huduma hospitalini hapo. Mwisho alisisitiza ushirikiano ili kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.



Tarehe 29/12/2021